JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# TAARIFA KWA UMMA

## MAFUNZO YA WASICHANA KATIKA TEHAMA [GIRLS IN ICT SPATIAL INNOVATORS] 2025

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inawaalika wanafunzi wasichana wanaosoma vyuo vikuu nchini, kushiriki katika mafunzo na shindano Wasischana katika TEHAMA Mafunzo na Mashindano ya **Girls in ICT Spatial Innovators.**

Shindano hili linalenga kuunda mawazo na dhana bunifu zaidi zinazohusiana na kaulimbiu ya maadhimisho ya Wasichana katika TEHAMA mwaka 2025 isemayo: **"Bridging all Divides for an Inclusive Digital Transformation"**

Mafunzo haya yanatoa fursa ya kipekee kwa wasichana kushiriki kikamilifu, kuonesha ujuzi wao na kufurahia ubunifu, uvumbuzi na ufanisi na hatimaye kufuzu kutengeneza suluhisho za kiteknolojia kwa changamoto za jamii.

**Vigezo vya Kushiriki:**

- Mwanafunzi wa kike Mtanzania anaesoma katika Chuo Kikuu;
- Ujuzi wa msingi wa Teknolojia ya Geospatial (Remote Sensing, GIS, GPS);
- Umri kuanzia miaka 18 hadi 24;
- Uanachama katika Vilabu vya Kidijiti ni lazima.

Washiriki wanatakiwa kuwasilisha maombi yao kwa njia ya mtandao kupitia kiunganisho kifuatacho https://digitalclubs.tz/get-started

**Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 07 Machi, 2025.**

TCRA inawahimiza wanafunzi wote wa kike wenye vigezo vilivyotajwa, kuchangamkia fursa hii adhimu kuonesha vipaji vyao kwenye Nyanja ya TEHAMA.

Kwa maswali yoyote tafadhali wasiliana na Dawati la Huduma kwa wateja la TCRA kupitia **0800008272** au kwa barua pepe: **dawatilahuduma@tcra.go.tz**

Imetolewa tarehe **21 Februari, 2025.**

Digitally Signed By JABIRI KUWE BAKARI
Fri Feb 21 23:55:44 EAT 2025

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
**Simu:** +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 **Nukushi:** +255 22 2412009-10
**Barua pepe:** barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, **Tovuti:** www.tcra.go.tz